


Thathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea

Mwongozo kwa wazazi na walezi

Thathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea ni thathmini ya nchi nzima ambayo huwasaidia walimu kutambua stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu za Kiingereza za kila mwanafunzi mwanzoni mwa shule ya chekechea.



Watoto huanza shule wakiwa na stadi mbalimbali za mapema za kusoma, kuandika na kuhesabu, maarifa na uelewa unaokuzwa kutokana na kuunganishwa na ulimwengu na watu wanaowazunguka. Thathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea inajumuisha kipengele cha kusoma na kuandika na kuhesabu na huwapa walimu taarifa kuhusu uwezo na mahitaji ya mwanafunzi binafsi.

Thathmini inawasaidia walimu kuunda programu za kufundisha na kujifunzia zinazojengwa juu ya kile ambacho wanafunzi wanajua. Walimu huketi na kila mwanafunzi mmoja mmoja, wakizingatia kile wanachoweza kufanya. Mtoto wako hahitaji kuijandaa au kusoma kwa ajili ya thathmini. Watoto wanapojoifunza viwango tofauti hakuna haja ya kuwa na wasiwas ikiwa mtoto wako hawezi kujibu maswali yote.

Mda mfupi baada ya thathmini, walimu watakuza taarifa kuhusu ujuzi, maarifa na uelewa ambao mtoto wako alionyesha wakati wa thathmini.

Thathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea inajumuisha wanafunzi wote. Ikiwa Kiingereza si lugha yako ya nyumbani au mtoto anahitaji marekebisho, wasiliana na shule yako kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi mtoto wako anavyoweza kusaidiwa.

| Thathmini ya kusoma na kuandika

Kazi za kusoma na kuandika zimeundwa ili kutambua kama wanafunzi wanaweza kuandika majina yao, kutambua sauti, herufi na maneno yanayofahamika, na kukumbuka maelezo kuhusu kitabu kifupi ambacho wamesomewa.

Wakati wa thathmini ya kujua kusoma na kuandika mwalimu atamuuliza mtoto wako maswali kama vile:

- 'Sikiliza maneno haya: map, tap. Je, unaweza kufikiria neno lingine ambalo lina mashairi?'
- '(baada ya kusoma kitabu kifupi) Je unaweza kuniambia kuhusu hadithi ambayo nimetoka kukusomea?'

Maswali haya huwasaidia walimu kuamua ikiwa mtoto wako anaweza kutambua maneno yanayofanana na kukumbuka maelezo kutoka kwa kitabu kifupi alichosomewa. Hizi ni ujuziujuzi muhimu zwa kusoma na kuandika ambao watoto watakuza katika mwaka wao wa kwanza shulenii.

| Thathmini ya kuhesabu

Majukumu ya kuhesabu yanahusiana na dhana za nambari za mapema na yameundwa ili kutambua jinsi mwanafunzi anavyoweza kuhesabu, nambari gani anaweza kutambua, iwe anaweza kuhesabu vitu, kuongeza au kutoa nambari ndogo; na kutambua mifumo inayojirudia.

Wakati wa thathmini ya kuhesabu, mwalimu atamuuliza mtoto wako maswali kama vile:

- 'anza kuhesabu kutoka moja na nitakuambia wakati wa kuacha'
- 'unaweza kuniambia hii ni namba gani?' (5)

Maswali haya yatawasaidia walimu kubaini kama mtoto anaweza kutambua nambari ya kuhesabu kuanzia moja na kendelea. Hizi ni ujuzi muhimu zwa kuhesabu ambao watoto watakuza katika mwaka wao wa kwanza shulenii.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Thathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea, wasiliana na shule ya mtoto wako.

Ikiwa unahitaji mkalimani, wasiliana na Huduma ya Ukalimani kwa simu kwa nambari 131 450. Wanaweza kupanga mkalimani katika lugha yako ili kusaidia mazungumzo na shule. Hautazwa kwa huduma hii.